KUPANDA MPUNGA KWA MBINU ZA KILIMO HAI

TOAM
Tanzania Organic Agriculture Movement

Kupanda mpunga kwa kutumia mbinu za kilimo-hai hukuhakikishia kiwango cha uzalishaji ulio endelevu. Kuchagua mbegu sahihi, usimamizi wa shamba na shughuli zinazofanyika baada ya mavuno ni muhimu ili upate mavuno mazuri.

Kulingana na Shirikisho la kimataifa la harakati za kilimo hai (IFOAM, 2008), Kilimo-hai kinafafanuliwa kuwa ni " mfumo wa uzalishaji ambao unaendeleza afya ya udongo, mifumo ya ikolojia na watu. Kilimo hiki hutegemea kwenye michakato ya ki-ikolojia, bioanuwai na mizunguko asilia ambayo inakubaliana na mazingira ya maeneo husika, badala ya kuingiza pembejeo ambazo zina athari mbaya. Kilimo hai kinajumuisha utamaduni, ubunifu na sayansi ili kunufaisha mazingira tunayoshirikiana na kukuza mahusiano ya haki na maisha bora kwa wote wanaohusika".

Kuchagua aina zinazofaa na mbegu nzuri

Kuchagua aina mpya

Mambo ya kuzingatia:

1. Kama ni aina ya ma-bondeni au milimani
2. Imeshajaribishwa eneo husika
3. Mbegu inayotumika mara nyingi
4. Mavuno mazuri

Kuchagua mbegu zako

Chagua mbegu zilizokomaa tu, zinazolingana afya yake na ambazo hazina ugonjwa

- Chagua aina ambazo zinafaa na zinatumika katika mazingira husika.
- Mpunga hujipevusha wenyewe. Hii inaruhusu kuchagua mbegu kutoka shambani kwako mwenyewe.
- Usipure mbegu ambazo zitatumika wakati wa kusia.
- Mavuno ya kiangazi ni chanzo kizuri cha mbegu bora.
- Tenga kilo 30 hadi 40 za mbegu kwa ajili ya kupanda hekta 1.

Kupima uhai wa mbegu na matayarisho ya mbegu

Kupima uhai wa mbegu

1. **Loweka mbegu**

Hesabu mbegu 100 na ziloweke kwenye maji kwa masaa 24

2. **Vundika**

Fungasha mbegu kwenye karatasi au kitambaa chenye unyevunyevu kwa siku 2

3. **Hesabu mbegu zilizochipua**

Hesabu mbegu zote zilizochipua na idadi hiyo iweke kwa asilimia ya 100.

Kabla ya mbegu kuchipua:

- Anza kutayarisha mbegu kabla ya mvua kuanza.
- Mbegu zinazotoka kuhifadhiwa miezi 3 au zaidi zinahitaji kwanza kupashwa joto kwenye jua kwa masaa 3.
- Ruhusu mbegu zipoe kabla ya kuziloweka kwa siku 1.
- Ondoa mbegu zinazoelea.
- Jaza mbegu nusu kiroba kwa ajili ya kuvundika kwa masaa 36. Kagua mbegu mara kwa mara ili joto lisipande sana kwenye jua.

Kuboresha mbinu za usimamizi



> Tengeneza matuta kupunguza upotevu wa udongo.
> Epuka usumbuaji wa ardhi usio wa lazima.
> Boresha rutuba na hifadhi ya udongo kwa kilimo mseto kwa kutumia mazao yatakayokuwa mbolea za kijani.
> Zuia upungufu wa virutubisho kwa kuongeza mbolea za kilimo hai na fosfeti ya mawe
> Zuia ushindani wa magugu na mbegu zake kuongezeka kwa kufanya palizi ya mara kwa mara kwa muda sahihi.

Kuchagua mfumo sahihi wa uzalishaji

Mfumo wa kilimo shadidi cha mpunga

Kumwagilia maji:
- Weka udongo kuwa na unyevunyevu, lakini usilowe mpaka wakati wa kutoa maua
- Usiongeze maji katika siku 25 za mwisho kabla ya kuvuna

Kupanda:
- Pandikiza miche ingali michanga (siku 8 hadi 12)
- Panda katika mfumo wa mraba wa sm 25x25



Kupalilia:
- Palizi ya kwanza: Siku 10 baada ya kupanda
- Palizi ya pili: ndani ya wiki mbili baada ya kwanza
- Palizi ya ziada: Mara 1 au 2 kabla ya kutoa maua

Kuweka mbolea:
- Ongeza mboji au mbolea wakati wowote inapowezekana

Mfumo wa Kilimo shadidi cha mpunga (SRI) ni mbinu kabambe yenye mafanikio inayosaidia kuongeza uzalishaji.

> Kurekebisha mfumo wa uzalishaji ili uendane na mazingira yaliyopo
> Kilimo mseto na kilimo cha mzunguko wa mpunga na mazao mengine.
> Kilimo mchanganyiko wa aina tofauti za mpunga, kila aina ikiwa na eneo lake

Utunzaji sahihi baada ya mavuno ili kupunguza upotevu

1. Kuvuna

2. Kukausha



3. Kupura na kufungasha

4. Kukoboa na kuhifadhi/kuuza

> Vuna pale tu mpunga utaka-pokuwa umekomaa.
> Kupanda aina mchanganyiko kunaweza kusababisha shamba moja likawa na viwango tofauti vya kukomaa.
> Tandaza nafaka zisilundikane wakati wa kukausha kuzuia kuvu.
> Tumia mashine sahihi za ku-koboa ili kuhakikisha asilimia kubwa ya punje za mchele zinatoka nzima.
> Mchele unatakiwa usiwe na makapi, mbegu za magugu na mawe ili kupata bei nzuri

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

Mchapishaji: TOAM kwa kushirikiana na FIBL. Kipeperushi hiki kinapatikana bure katika lugha za Kiswahili na Kiingereza kwenye tovuti: www.organic-africa.net/www.kilimohai.or.tz. Kimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Dk. George M. Kiama (excelmercantile@yahoo.com). Tunawashukuru shirika la Uswisi linaloshughulikia maendeleo na ushirikiano (Swiss Agency for Development and Cooperation) Dar es Salaam kwa msaada walioutoa kufanikisha tafsiri ya kipeperushi hiki. This flyer is freely available for download in both English and Swahili from www.organic-africa.net / www.kilimohai.or.tz.